**TAARIFA YA MKURUGENZI MKUU WA MAMLAKA YA SERIKALIMTANDAO (e-GA) MHA. BENEDICT NDOMBA, KWA NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA, MHE. RIDHIWANI JAKAYA KIKWETE, WAKATI WA KUFUNGA KIKAO KAZI CHA NNE (4) CHA MWAKA CHA SERIKALI MTANDAO FEBRUARI 8, 2024 KATIKA UKUMBI WA AICC ARUSHA.**

***Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb);*** *Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora,*

***Ndg*****. Xavier Daudi*****;*** *Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora,*

***Mhe. Emmanuela Mtatifikolo Kaganda,*** *Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Arusha,*

***Dkt. Jasmine Tiisekwa;*** *Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA),*

***Bw. Said Seif Said;*** *Mkurugenzi Mtendaji Wakala ya Serikali Mtandao Zanzibar (e-GAZ),*

***Wakurugenzi wa Halmashauri, Mashirika na Taasisi Mbalimbali,***

***Wakuu wa Idara za TEHAMA na Watumishi kutoka Taasisi mbalimbali,***

***Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, na Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao,***

***Waandishi wa Habari;***

***Mabibi na Mabwana;***

***Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;***

Awali ya yote, namshukuru mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukutana hapa leo katika hafla hii fupi ya kuhitimisha Kikao Kazi hiki cha nne (4) cha mwaka cha Serikali Mtandao.

Kipekee nikushukuru sana **Mhe. Naibu Waziri,** kwa kukubali na kuitikia wito wetu wa kushiriki nasi hapa leo. Natambua kuwa, unayo majukumu mengine muhimu ya kitaifa, lakini umeweza kutenga muda ili ushiriki nasi katika kikao kazi hiki muhimu cha Serikali Mtandao. Uwepo wako hapa ni ishara tosha kuwa, Wizara yako imedhamiria kuhakikisha kuwa jitihada za Serikali Mtandao zinakua na kuimarika. Tunakushukuru sana na nikukaribishe tena kwa mara nyingine.

Nitoe shukrani zangu za dhati kwa Viongozi na Watumishi wote wa Serikali, Mashirika na Taasisi za Umma, sekta Binafsi na Waandishi wa Habari kwa kushiriki nasi kwa siku zote tatu (3) za Kikao Kazi hiki. Tunatambua kuwa, mafanikio ya Serikali Mtandao yanatokana na ushirikiano wa wadau wote, ikiwemo Serikali na sekta binafsi. Ushirikiano huu ndio umeleta mapinduzi makubwa katika matumizi ya huduma za Serikali Mtandao katika kipindi cha takriban miaka 10 iliyopita, kama ilivyobainishwa na kuelezwa kwa kina wakati wa Kikao Kazi hiki.

Kwa niaba ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), niwashukuru washiriki wote mliohudhuria Kikao Kazi hiki, kilicholenga kuwakutanisha wadau mbalimbali wa Serikali Mtandao, ambapo tulijadiliana kuhusu mikakati mbalimbali ya kuendeleza na kutumia

huduma za Serikali Mtandao, kubainisha changamoto zilizopo na kuziwekea mikakati madhubuti ya kukabiliana nazo.

Aidha, niwapongeze kwa umakini, utulivu na usikivu wenu wakati wote wa Kikao Kazi hiki, na niwashukuru kwa michango mliyotoa kwa ajili ya kuendeleza na kuimarisha jitihada za Serikali Mtandao.

Kwa ruhusa yako **Mhe. Naibu Waziri,** Naomba niwatambue wadhamini wote wa kikao kazi hiki cha 4 cha Serikali Mtandao, ambao wamechangia mafanikio ya kikao hiki kwa asilimia kubwa sana. Aidha, e-GA inathamini sana michango yenu na ushirikiano mliotupatia wakati wote wa maandalizi ya kikao hiki, na muhimu zaidi mmeshiriki nasi kuanzia mwanzo hadi wakati huu tunapohitimisha kikao hiki. Niwaombe tuendelee kushirikiana zaidi katika jitihada mbalimbali za kuimarisha Serikali Mtandao.

**Mhe. Naibu Waziri;** Kikao kazi hiki kiliongozwa na kaulimbiu isemayo ***"*Uzingatiaji wa Sera, Sheria, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa Ubadilishanaji Salama wa Taarifa*"* *(Compliance to e-Government Policies, Laws, Standards and Guidelines for Secure Electronic Data Exchange)***.

Kaulimbiu hii ililenga kusisitiza na kuzikumbusha Taasisi za Umma kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao, katika ujenzi wa miundombinu na mifumo ya TEHAMA katika taasisi zao. e-GA tunaamini kuwa, ikiwa miradi na mifumo ya TEHAMA itazingatia ipasavyo Sera, Sheria, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao itasaidia kupunguza urudufu wa mifumo, kurahisisha taasisi za umma kubadilishana taarifa pamoja `na kusaidia kuokoa fedha za umma kwa kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali.

**Mhe. Naibu Waziri;** Katika kipindi cha siku tatu za kikao Kazi hiki, mada mbalimbali zinazohusu Serikali Mtandao ziliwasilishwa na kujadiliwa kwa kina. Mijadala ya Mada hizo zilihusu namna ambavyo Taasisi za Umma zimekuwa zikitekeleza Jitihada za Serikali Mtandao. Vilevile, mada hizo zilibainisha namna ambavyo Serikali Mtandao imesaidia kuongeza tija na ufanisi wa utendaji kazi katika taasisi za umma na utoaji wa huduma kwa wananchi.

Kupitia mijadala ya washiriki, Mamlaka imepokea maoni na ushauri kuhusu maboresho ya maeneo mbalimbali ya Serikali Mtandao, na kuweka maazimio. Tunaahidi kuyafanyia kazi maazimio yote pamoja na kupokea maelekezo yako, ambayo utayatoa hapa leo.

**Mhe. Naibu Waziri;** Mamlaka inaahidi kuendeleza ushirikiano huu mzuri uliopo miongoni mwa Taasisi za Umma, ambao ni wadau muhimu wa serikali mtandao. Tutaendelea kushirikiana katika kutatua changamoto zilizopo katika jamii yetu, ikiwemo kuboresha utendaji kazi katika Taasisi za umma na utoaji wa huduma kwa umma. Nikuhakikishie **Mhe. Naibu Waziri** pamoja na washiriki wote hapa kuwa, Mamlaka itaendelea kushirikiana na Taasisi za Umma katika kubuni, kusanifu na kujenga Mifumo mbalimbali ya TEHAMA itakayosaidia kutatua changamoto zilizopo katika jamii yetu, na kuiwezesha Serikali kutoa huduma kwa wananchi kwa urahisi, haraka na kwa gharama nafuu zaidi.

**Mhe. Naibu Waziri;** pamoja na mikakati mbalimbali ambayo tumejiwekea kama Mamlaka kwa lengo la kuhakikisha Serikali Mtandao inaimarika, lakini naomba nitumie nafasi hii kukuomba **Mhe. Naibu Waziri,** umfikishie salamu na shukrani zetu za dhati **Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa usimamizi wake mahiri na dhamira yake ya kuijenga serikali kidijitali. Dhamira yake na maelekezo

anayoyatoa kwetu mara kwa mara yamekuwa chachu katika utendaji kazi wetu, tukiwa wasimamizi wa utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao, tutahakikisha Mamlaka inasadia kufikia azma yake ya kuijenga Serikali ya Kidijitali.

**Mhe. Naibu Waziri,** niiombe Serikali kupitia Wizara yako, kuendelea kuweka mazingira wezeshi kwa Mamlaka ya Serikali Mtandao ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na weledi wa hali ya juu katika kuhakikisha Serikali ya kidijitali inafanikiwa hapa nchini.

Kwa mara nyingine tena, nikushuru **Mhe. Naibu Waziri** pamoja na washiriki wote mliohudhuria Kikao Kazi hiki, na niwakaribishe tena katika Kikao kingine kama hiki wakati mwingine na msisite kuhudhuria.

**Mhe. Naibu Waziri;** Baada ya kusema hayo, naomba sasa nimkaribishe Makamu wa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao **Dkt. Jasmine Tiisekwa** ili aweze kutoa salamu za Bodi.

***Asanteni sana kwa kunisikiliza***

***“Karibu tuijenge Serikali Kidijiti”***